

# Jua Hatari Yako kwa Kuugua Sana Kutokana na COVID



## **Watu wanaougua sana kutokana na COVID wanaweza kuhitaji kutunzwa hospitalini. Hata wanaweza kufa.**

Kuendelea kupata vyanjo vipyta vya COVID ni njia bora ya kujilinda na kuugua sana kutokana na COVID.

Baadhi ya watu wana hatari zaidi kuliko wengine ya kuugua sana kutokana na COVID - hata ikiwa wamepewa chanjo.

## **Sababu zinazohatarisha watu zaidi kuugua sana kutokana na COVID**

### **Umri mkubwa**

Hatari ya ugonjwa kali kutokana na COVID inazidi na umri, hasa kwa watu wenye miaka 50 na zaidi.


### **Mfumo wa ukinga uliodhoofika**

Kwa sababu ya hali ya kiafya au dawa inayodhoofisha mfumo wa ukinga, kama kemikali za chemotherapy au corticosteroids.

### **Masuala fulani ya afya**

Masuala fulani ya afya huongeza hatari yako zaidi kuliko mengine. Na ukiwa na masuala zaidi, hatari yako itaongezeka. Masuala ya afya ya kawaida yanayoongeza hatari yako yanatia ndani:

- Hali za moyo
- Sukari
- Pumu na hali nyingine za mapafu
- Saratani (Kansa)
- Hali za figo au ini
- Kuwa na uzito kipita kiasi au mnene sana



**Hayo si masuala yote ya afya yanayohusishwa na kuongeza hatari ya ugonjwa kali kutokana na COVID. Ongea na daktari yako au mtoaji wa matibabu kuhusu masuala yako ya afya ili kuelewa hatari yako.**

## **Matibabu yameyoidhiniwa au kubaliwa na FDA yanapatikana ili kusaidia kuzuia ugonjwa kali**

Ikiwa una hatari zaidi kuugua sana, unahitaji kuanzisha matibabu kwa COVID mara moja baada ya dalili zinapoanza.

**Usingoje.** Ni muhimu kupimwa haraka ukiwa na dalili za COVID. Matibabu ya agizo la daktari yanahitaji kuanzishwa katika siku ambazo dalili zinapoanza.

Hata ikiwa dalili zako si kali, kutibu COVID yako mapema na dawa inayoagizwa na daktari au mtoaji mwengine wa matibabu ambaye ameidhiniwa inaweza kufanya ambukizo lako lisiwe kali na kukusaidia usilazwe hospitalini. Inaweza kuokoa uhai wako.

**Ongea na daktari yako au mtoaji wa matibabu kuhusu hatari yako ya kuugua sana  
kutokana na COVID.**

**Jifunze zaidi kwenye [cdc.gov/covidtreatment](https://cdc.gov/covidtreatment)**